www.ippmedia.com

# Alasiri Online

Alhamisi Aprili 18, 2019

Tanzani 500/- Kenya 50/-



# Q CHIEF ACHOMOA TIKISA

## AMINI WABEBANA NA LINAH



# Q CHIEF ACHOMOA TIKISA

Na Mary Kadoke

BAADA ya kutamba na ngoma ya Chuma Kisamvu, Q Chillah maarufu kama Q Chief ameachia tena 'Tikisa'.

Akizungumza na Alasiri Online amesema dhamira ya kuachia ngoma hiyo ni kuburudisha mashabiki zake kwa maudhui mbalimbali tofauti na zile alizoachia mwanzo.

"Si kila siku nitatoa nyimbo za manung'uniko, Tikisa inachezeka," amesema.

"Nilitaka niwe tofauti kidogo na ngoma zangu za kutendwa, naimani Tikisa itafanya vizuri kwa sababu asilimia kubwa inahamasisha kucheza," amesema.

Ni miezi minane sasa imepita tangu aachie 'Chuma Kisamvu' iliyotoka Julai mwaka jana.

Kazi hii imepikwa katika studio za Bongo Records na video kuandaliwa jijini Dar es salaam.

# Gigy amwaga mboga kweupee

Na Mary Kadoke



GIGY amemrushia lawama lawama mzazi mwenzake Mo J akieleza kuwa haoni mantiki ya mwanaye Myra (1) kuwa na baba kwani ndiye anayemhudumia kwa kila kitu.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online amesema Mo amekuwa mtu wa kuibuka na kuulizia hali ya mtoto tu bila kutoa chochote, hasa pale anapoona Gigy karusha picha akiwa na mrithi wa Mo, Hunchy Huncho. "Nimeshasema na ninaendelea kuisema mwanangu hana baba, mwanangu hawezi kuwa na baba ambaye hajui mwanaye anakula nini, anavaa nini au anaishi vipi," amesema

"Huchangii chochote mpaka unapoona nimepost picha ya boyfriend ndio unaibuka?" ameongeza.

Aidha Alasiri Online ilimsaka Mo ili kujibu tuhuma hizi na alichokisema ni: "Mawasiliano na mzazi mwenzangu yapo sawa na kuhusu mtoto najitahidi kutoa matumizi mara kwa mara." Hii si mara ya kwanza Gigy kutoa lawama za mtoto wake kutohudumiwa, mwaka jana aliwahi kulalamika kuachiwa buku na Mo kama pesa ya matumizi ambayo haikuwa inakimu mahitaji yake kama mama na kwa mtoto wao.

## HABARI KITAIFA

# AMINI WABEBANA NA LINAH



Na Anaeli Mbise

MSANII wa kizazi kipya Amini akishirikiana na Linah wametoa ngoma mpya inayokwenda kwa jina la Nimenasa.

Akizungumza na Alasiri Online, mwanamuziki Amini amesema kuwa ameamua kumshirikisha Linah kutokana na sauti nzuri ya chorus aliyonayo na ya kumtoa nyoka pangoni.

"Nilimshirikisha msanii mwenzangu kutokana na sauti kali aliyonayo na hakika ameitendea vizuri katika ngoma hii mpya," amesema Amini. Kadhalika mwanamuziki huyo amesema ujumbe unaopatikana katika ngoma hiyo unazungumzia mapenzi namna ambavyo mtu amenasa kwa mpenzi wake.

Kwa upande wake mwanamuziki Linah amesema kuwa amefurahia kushirikiana na Amini kwa sababu inajenga uhusiano mzuri miongoni mwa wasanii.

## SR FEY ATULIZA MAHABA

Na Mary Kadoke

KUNGWI wa Instagram na mwanamuziki, Sr Fey, amempata mrithi wa huba lake la mwanzo alilowekeza kwa, Holy Star, ambaye ni muigizaji Petitman Wakuache.

Hii ni baada ya kuvujisha video kupitia ukurasa wake wa Instagram @fey_tanzania wakiwa wanamwagiana mahaba motomoto.

Video hiyo aliipa maelezo, "Kwa nini nijibanebane buana."


Hata hivyo jitihada za kumsaka Fey kwa njia ya simu alishia kusema hawezi zungumzia suala hilo kwa sasa.

Wawili hawa awali walikuwa katika mahusiano ya ndoa ambazo zilivunjika na hakuna upande uliowahi kutoa sababu ya kuachana kwao.

Petit alikuwa mume wa dada wa Diamond Platnumz, Esma Platnumz waliobahatika kupata mtoto mmoja Taraj (4) na Fey aliwahi kuolewa na Holystar ambaye baadaye waliachana.

Ukungwi wa Fey huufanyia katika ukurasa wake wa Instagram kufunda watu usafi, mahusiano na mapishi hii yote ni katika kuokoa ndoa zao.

Ngoma yake iliyowahi kumuweka mjini ni Kaja Mwenyewe.





# Lady Jay Dee kweli komandoo

**Na Anaeli Mbise**

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya Lady Jay Dee, hataki mbwembwe za kuwa na mabaunsa kama wafanyavyo baadhi ya wasanii.

Akizungumza na Alasiri Online, Jay Dee amesema kuwa haoni sababu za kukodi mabaunsa kwa sababu ni kujiingiza katika gharama ambazo hazina msingi.

"Mimi mwenyewe ni komandoo hivyo sioni sababu ya kuwa na mabaunsa, katika shughuli zangu za muziki ninajitosheleza," anasema Jay Dee.

Mwanamuziki huyo amesema katika shughuli zake za muziki amekuwa akizunguka na wasaidizi wachache na siyo mabaunsa wa kumlinda.

Msanii huyo kwa sasa ana kibao kipya alichokipa jina la 'I don't Care' ambacho anatarajia kukitambulisha wiki ijao.

# Tobi One amsaka Lavalava



**Na Anaeli Mbise**

MSANII chipukizi Tobi One, kutoka jijini Mwanza, amesema anatamani siku moja afanye kazi na Lavalava.

Akizungumza na Alasiri Online, Tobi amesema kuwa anajiamini katika kazi na hivyo kushirikiana na Lavalava wa WCB itakuwa jambo muhimu ili kukuza zaidi kipaji.

"Ninapenda sana uimbaji wake ila sijui itawezekana kumpata na kumshirikisha katika nyimbo zangu? Kwa kweli nina imani sana kufanya naye kazi," amesema Tobi.

Tobi amesema kuwa anaamini wasanii wakubwa wako wengi, lakini anavutiwa zaidi na Lavalava na kwamba iko siku watakutana ili amuombe ampige tafu katika nyimbo zake.

"Nina nyimbo nyingi tu ambazo sijazirekodi, hivyo ninawatafuta wasanii kama Lavalava niwashirikishe ili niweze kuwa juu," amesema Tobi.